**MULIKA Na. 40(1) 2021 (42-56)**

# Ulinganishi wa Ngeli za Nomino za Kipemba na Kingazija

*Sauda Uba Juma*[1]

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

## Ikisiri

Makala haya yanachunguza ulinganishi wa ngeli za nomino za Kipemba na Kingazija ili kubaini namna zinavyofanana na kutofautiana. Makala haya ni sehemu ya utafiti mpana uliofanywa wa kulinganisha kiisimu Kipemba na Kingazija kwa lengo la kubaini uhusiano wa kimnasaba uliopo miongoni mwake. Ulinganishi wa ngeli za nomino umejikita kwenye viambishi katika maumbo ya umoja na wingi. Data iliyotumika katika utafiti uliozaa makala haya ilikusanywa uwandani kupitia mbinu za hojaji na mahojiano. Ulinganishi wa ngeli za nomino unaweza kufanywa kwa kutumia mikabala mbalimbali kulingana na wanazuoni tofauti waliojaribu kuainisha ngeli za nomino. Hata hivyo, katika makala haya ulinganishi huo umefanywa kwa kuegemea kigezo cha kimofolojia. Lengo ni kubaini namna maumbo ya viambishi vya umoja na wingi vya Kipemba na Kingazija yanavyofanana na kutofautiana. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba Kipemba na Kingazija zinashabihiana katika mfumo wake wa ngeli za nomino. Hali hii inaashiria kwamba lahaja hizi zimetokana na lugha-mame moja.

## 1.0 Utangulizi

Makala haya yanakusudia kulinganisha mfumo wa ngeli za nomino za Kipemba na Kingazija ili kuona namna zinavyofanana na kutofautiana. Lengo la kufanya hivi ni kutaka kuthibitisha au kukanusha hoja kwamba lahaja za Kipemba na Kingazija zinazotokana na lugha chanzi moja au ni lugha ambazo hazihusiani. Hii imetokana na misigano miwili kinzani iliyopo miongoni mwa wanazuoni kuhusu kadhia hii. Upande mmoja unadai kuwa Kingazija ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili. Huu unawakilishwa na wanazuoni kama Chiraghdin na Mnyampala (1977), Kipacha (2003) na Massamba (2017). Upande wa pili ni mtazamo kuwa Kingazija si miongoni mwa lahaja za Kiswahili bali ni lugha inayojitegemea. Huu unawakilishwa na Nurse na Spear (1985), Nurse (1989) na Nurse na Hinnebusch (1993). Misigano ya pande hizi mbili ndiyo iliyotupa mshawasha wa kuzilinganisha ngeli za nomino za Kipemba na Kingazija ili kubaini namna zinavyoshabihiana na kuachana kwake.

Ngeli za nomino ni kipengele kimojawapo cha kiisimu kinachotumika katika ulinganishi wa lugha mbili au zaidi. Kipengele hiki kinahusu makundi mbalimbali ya majina, hasa katika lugha za Kibantu, ambayo kila moja huwa na sifa tofauti na

[1] **Baruapepe:** chudam017@gmail.com.

jingine kulingana na vigezo vya uainishaji ambavyo vimetumika (Massamba, 2004). Hii ina maana kuwa ngeli za nomino huweza kugawanywa katika makundi mbalimbali kulingana na vigezo anuwai vilivyotumika. Nao Khamis na Kiango (2002) wanadai kuwa nomino za Kiswahili zina tabia kadhaa zinazozitambulisha na kuzitofautisha na aina nyingine za maneno. Nomino yoyote iliyomo ndani ya lugha ya Kiswahili na yoyote iingiayo, haina budi kuingia katika ngeli fulani. Bila shaka, nomino ambazo maumbo yake yanaruhusu kutambua ngeli, ni zile ambazo zinaruhusu viambishi ngeli ambavyo vinatangulia mizizi ya nomino hizo katika maumbo yake.

Kutokana na hali hii, mara nyingi lugha zote ulimwenguni zenye mfumo wa ngeli, huwa na idadi mahususi ya ngeli. Hali huu hutokea pia katika lugha mbalimbali za Kibantu zinazotumia mfumo huo wa kupachikwa viambishi mbalimbali vinavyojulikana kama viambishi vya ngeli. Aidha, kila lugha ina idadi maalumu ya ngeli, ambapo kwa wastani, lugha nyingi zina ngeli zisizopungua 10 na zisizozidi 20 (Kihore *na wenzie*, 2012). Makala haya yamegawika katika sehemu zifuatazo: utangulizi, kiunzi cha nadharia, mbinu, uianishaji wa ngeli za nomino, mfumo wa ngeli za Kipemba na Kingazija, na hitimisho.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ya Isimu Historia-Linganishi iliyoasisiwa na Jones (1786) imetumika katika uchambuzi wa data za makala haya. Jones alihudhurisha nadharia hii katika mhadhara wake uliohusu lugha ya Kisanskriti ambapo alibaini kuwa Kiyunani, Kilatini na Kisanskriti zinaelekea kuwa na chimbuko moja. Nadharia hii ina misingi mikuu miwili. Mosi, ulinganishi wa kisinkronia ambao unalinganisha lugha mbili au zaidi kama zilivyo hivi sasa ili kuona jinsi zinavyofanana na kutofautiana. Pili, kuzichunguza lugha kidikronia ambapo lugha mbili au zaidi zinaweza kuchunguzwa maendeleo yake katika kipindi mahususi cha kihistoria. Aidha, wako wanazuoni ambao waliiboresha nadharia hii. Wanazuoni hao wanatofautiana na mwanzilishi kwa kuiboresha kwa kuwa ndani ya nadharia hii kuliibuka mbinu linganishi kama ilivyopendekezwa na Anttila (1972) na takwimu leksika kama ilivyopendekezwa na Swadesh (1952). Katika kuitumia mbinu hiyo vigezo vifuatavyo ni lazima vizingatiwe:

Mosi, kuchunguza msamiati wa msingi katika lugha zinazolinganishwa. Msamiati huu ni ule unaohusu vitu vya kawaida katika mazingira ya wasemaji wa lugha zinazohusika, vitu vilivyo vya asili katika mazingira hayo, majina ya viungo vya mwili na shughuli za kila siku za jamii inayohusika (Anttila, 1972). Pili, kuchunguza mfumo wa maumbo ya maneno ya lugha hizo. Tatu, kuchunguza mfumo wa sauti katika lugha zinazoshughulikiwa. Nne, kuchunguza miundo ya maneno ya lugha zinazohusika. Tano, kuchunguza mfumo wa uainishaji wa ngeli. Sita, kuchunguza vipengele vingine muhimu kama vile mkazo au toni vya lugha zinazochunguzwa. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili ililinganishwa na lugha za Kiruuri, Kizuulu na Gikuyu kwa kutumia vipengele hivyo vya kiisimu (Massamba, 2017). Pamoja na kuwa lugha hizo zilizolinganishwa zina maelfu ya umbali wa maili au kilomita kutoka lugha moja hadi nyingine. Hata hivyo, matokeo

yanaonesha kwamba zinatokana na mame-lugha moja. Hivyo, katika makala haya, tumetumia mbinu hii kulinganisha kipengele kimoja cha kiisimu ambacho ni ngeli za nomino za Kipemba na Kingazija kwa minajili ya kubaini jinsi zinavyofanana na kuachana kiisimu.

## 3.0 Methodolojia

Data za utafiti huu zimekusanywa uwandani katika maeneo ya Pemba na Ngazija. Maeneo yaliyohusishwa na utafiti huu katika kisiwa cha Pemba yamechaguliwa kwa sababu wazungumzaji wake wanatumia zaidi lugha zao kuliko Kiswahili sanifu hasa wanapokuwa katika mazingira yasiyo rasmi (Juma, 2011). Vijiji vilivyohusishwa katika utafiti huu ni Mwambe na Shamiani. Kwa mujibu wa tafiti zilizotangulia, hivi ni miongoni mwa vijiji ambavyo wazungumzaji wake hadi hii leo bado wanaendelea kuitumia lahaja yao ya Kipemba halisi (Juma, 2012) na (Juma, 2019). Kwa upande wa Ngazija maeneo yaliyohusika ni Moroni, Bangwakuni na Itsinkudi. Maeneo haya yamechaguliwa kwa sababu ndiyo yenye wazungumzaji wazawa ambao wanazungumza Kingazija cha asili.

Tulitumia mbinu ya hojaji yenye orodha ya maneno 200 ambayo ni msamiati wa msingi uliojumuisha kategoria mbalimbali za maneno. Msamiati huo uliandaliwa kutoka maktabani kwa kuzingatia mapendekezo ya Swadesh (1952) ya jinsi ya kuandaa msamiati wa msingi ambao ulihusu majina ya sehemu za mwili, maumbile ya asili, vitenzi vya asili, majina ya namba n.k. Maneno hayo yaliandikwa kwa lugha ya Kiswahili na visawe vyake viliandikwa kwa Kipemba na Kingazija. Hivyo, maneno hayo ambayo yalitokana na msamiati wa msingi, ndiyo yaliyotumika kulinganisha mfumo wa viambishi ngeli wa Kipemba na Kingazija. Kwa ujumla, mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata msamiati wa msingi uliochambuliwa ambao ulitumika kulinganisha viambishi mbalimbali vya ngeli za Kipemba na Kingazija vilivyotokea katika maumbo ya maneno hayo. Mbinu hii ilitumika kwa wale tu wanaojua kusoma na kuandika Kiswahili sanifu. Watoataarifa waliojaza hojaji ni: walimu 4 na wanafunzi 6 kutoka Pemba, na mwalimu 1[2] na wanafunzi 9 kutoka Ngazija, na kufanya jumla ya watoataarifa kuwa 20.

Mbinu ya mahojiano ilitumika kwa minajili ya kupata taarifa mbalimbali za kiisimu ambazo zilimsaidia mtafiti kupata data za mfumo wa maumbo ya maneno. Mbinu hii ilitusaidia kuthibitisha msamiati wa msingi ulikaokusanywa katika hojaji kabla ya uchambuzi. Katika kuitumia mbinu hii, tulijadiliana na wazee kuhusu masuala mbalimbali yakiwamo ya kihistoria ya wazungumzaji wa Kipemba na Kingazija pamoja na vikundi vya walimu na wanafunzi kutoka katika maeneo husika. Lengo lilikuwa kuchunguza jinsi maneno yanavyotamkwa katika matumizi ya viambishi ngeli. Aidha, kupitia vikundi hivyo tulijadili msamiati wa msingi ili kuhakiki ukubalifu wa data zilizokusanywa. Katika kuzitumia mbinu

[2] Mwalimu pekee anayefundisha Kiswahili Ngazija nzima.

hizo, wakati mwingine maneno ya Kifaransa[3] yalitumika pale ilipoonekana kuwapo na ulazima wa kuyatumia katika Kingazija. Hii ni kwa sababu Kifaransa ndiyo lugha rasmi inayotumiwa katika kisiwa cha Ngazija ambapo ilirahisisha mawasiliano. Hivyo, tulilazimika kuwa na mkalimani aliyeweza kufasiri lugha ya Kiswahili, Kingazija na Kifaransa hasa kwa wale ambao hawakuifahamu vizuri lugha ya Kiswahili. Aidha, mtafiti alilazimika kutumia kinasasauti kurekodi mazungumzo mbalimbali yaliyojadiliwa katika vikundi vilikavyohusika.

## 4.0 Uainishaji wa Ngeli za Nomino

Uainishaji wa ngeli za nomino ni utaratibu unaotumika katika kuzipanga nomino za lugha kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya kisarufi (Kihore *na wenzie*, 2012). Kwa ujumla, vigezo hivyo tunaweza kuvigawa katika makundi ambayo yanasimamia misingi mikuu minne. Misingi hiyo ambayo imekuwa ikitumika ni: kwanza, kutumia viambishi vya nomino. Pili, kutumia jozi ya viambishi vya umoja na wingi. Tatu, kutumia kiambishi cha upatanishi wa kisarufi na mwisho kutumia kiambishi cha nomino cha upatanishi wa kisarufi. Kila kigezo kilichobainishwa kina umuhimu na kasoro zake. Hata hivyo, si lengo letu katika makala haya kupitia na kuchambua kila kigezo cha uainishaji wa ngeli kiundani. Tulichofanya ni kutumia kigezo cha kimofolojia pekee ambacho kimeweza kutuongoza kuzibainisha ngeli za Kipemba na Kingazija pamoja na kuzilinganisha,na kuona jinsi zinavyofanana na kutofautiana.

## 4.1 Uainishaji wa Ngeli za Nomino za Kipemba na Kingazija kwa Kigezo Kimofolojia

Katika kigezo hiki, ngeli hutambulishwa kwa kupachikwa viambishi vinavyofanana mwanzo wa nomino. Kwa maana hiyo, nomino zilizobeba viambishi vya mwanzo vilivyo sawasawa huwekwa katika kundi la ngeli ya aina moja. Katika Kiswahili na hata lugha nyingine za Kibantu, viambishi awali vya nomino kwa kawaida hufuatia shina la nomino husika. Shina linajumuisha mzizi wa neno pamoja na irabu ishilizi. Mara nyingi nomino huwa na viambishi vinavyofanya kazi mbalimbali pamoja na sehemu ya mzizi wa neno. Mzizi ni sehemu ya msingi katika maumbo ya maneno kwa sababu huwa hauathiriwi wala haubadilikibadiliki kutokana na mchakato wa upachikwaji wa viambishi mbalimbali. Hivyo, kiambishi kinachotumiwa kuainisha ngeli kinaitwa kiambishi ngeli.

Katika utumiaji wa kigezo hiki, ngeli za Kiswahili huainishwa katika makundi mbalimbali kwa kuonesha umoja na wingi. Hata hivyo, si nomino zote katika Kiswahili zinaonekana kubeba viambishi vya ngeli. Aghalabu, katika Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu, baadhi ya maneno huwa hayana viambishi ngeli. Vilevile, katika uainishaji wa ngeli kimofolojia, mara nyingine nomino fulani huweza kufuata utaratibu wa kutumia kigezo cha kisintaksia au kisemantiki. Kwa mantiki hiyo, nomino inaweza kubainika katika ngeli fulani kimofolojia ikawa

---

[3] Maneno ya Kifaransa yalitumika kuondoa mkanganyiko pale ambapo neno la Kiswahili sanifu halikueleweka katika Kingazija.

katika ngeli nyingine kisintaksia au kisemantiki. Sanjari na utaratibu huo wa kubainisha ngeli kimofolojia, baadhi ya nomino huwa na viambishi vinavyofanana ingawa vinatofautiana ngeli. Aidha, kuna nomino ambazo hazina viambishi lakini zinaingia katika ngeli fulani. Hebu sasa tubainishe na kulinganisha ngeli za nomino za Kipemba na Kingazija kwa kutumia kigezo cha kimofolojia.

**5.0 Mfumo wa Ngeli za Nomino za Kipemba na Kingazija**

Tumeshadokeza hapo awali (taz. 2.0) kuwa lugha mbili au zaidi zinaweza kulinganishwa kwa kutumia vigezo mbalimbali vya kiisimu. Lengo la kutumia vigezo hivyo ni kutaka kujua kama lugha hizo zinatokana na mame-lugha moja au la. Kwani, bila shaka baada ya ulinganishi huo tunaweza kubaini namna lugha hizo zilivyofanana na kutofautiana. Hivyo, katika makala haya, tumezibainisha na kuzilinganisha ngeli za nomino za Kipemba na Kingazija ili kuona jinsi zinavyolandana na kutofautiana. Tuchunguze mifano katika Jedwali Na. 1:

**Jedwali Na. 1: Ulinganishi wa Ngeli za Nomino za Kipemba na Kingazija**

| **Ngeli** | **KiNG.** | **Kipemba** | **Kingazija** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|---|---|
| NG. 1 | m/n[4]-<br>mu<br>mw | **n**-tu | **m**-ndru | mtu |
| | | **mu**-umini | **mu**-umini | muumini |
| | | **mw**-anafuzi | **mw**-azioni | mwanafunzi |
| | | | | |
| NG. 2 | wa- | **wa**-tu | **wa**-ndru | watu |
| | | **wa**-waumini | **wa**-umini | waumini |
| | | **wa**-nafuzi | **wa**-nazioni | wanafunzi |
| | | | | |
| NG. 3 | m/n-<br>mu-<br>mw- | **n**-ti | **m**-ri | mti |
| | | **mu**-ndu | **mu**-ndru | panga |
| | | **mw**-ezi | **mw**-ezi | wezi |
| | | | | |
| NG. 4 | mi- | **mi**-ti | **mi**-ri | miti |
| | | **mi**-ndu | **mi**-ndru | mapanga |
| | | **mi**-ezi | **me**-zi | miezi |
| | | | | |
| NG. 5 | ji-<br>Ɵ-<br>gi-<br>di-<br>dzi- | **ji**-bwe | **Ɵ**-bwe | jiwe |
| | | **Ɵ**-shikio | **Ɵ**-shishiyo | sikio |
| | | **Ɵ**-jani | **Ɵ**-wani | jani |
| | | **gi**-no | **dzi**-nyo | jino |

[4] Matumizi ya 'n' badala ya 'm' katika Kipemba.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | dj/ja- | **di**-cho | **dzi**-tso | jicho |
| | | **ja**-bali | **dja**-bali | jabali |
| | | | | |
| NG. 6 | ma- | **ma**-bwe | **ma**-we | mawe |
| | | **ma**-shikio | **ma**-shishiyo | masikio |
| | | **ma**-jani | **ma**-ni | majani |
| | | **me**-no | **ma**-nyo | meno |
| | | **ma**-cho | **ma**-tso | macho |
| | | **ma**-jabali | **ma**-djabali | majabali |
| | | | | |
| NG. 7 | ki-<br>ky-/sh-<br>ha-<br>hi-<br>shi- | **ki**-buno | **shi**-wuno | kiuno |
| | | **ch**-akulya | **sh**-ahula | chakula |
| | | **ky**-uma | **sh**-uma | chuma |
| | | **kya**-nwa | **ha**-nywa | kinywa |
| | | **ki**-chwa | **hi**-tswa | kichwa |
| | | **ki**-yazi | **shi**-yazi | kiazi |
| | | | | |
| NG. 8 | vy-/zu<br>vi-<br>zi-<br>za- | **vya**-kulya | **za**-hula | vyakula |
| | | **vyu**-ma | **zu**-ma | vyuma |
| | | **vi**-buno | **zi**-wuno | viuno |
| | | **vi**-nywa | **za**-nwa | vinywa |
| | | **vi**-chwa | **zi**-tswa | vichwa |
| | | **vi**-yazi | **zi**-yazi | viazi |
| | | | | |
| NG. 9 | n- | **ng**-ozi | **ng**-ozi | ngozi |
| | | **ny**-umba | **ny**-umba | nyumba |
| | | **nj**-aa | **nd**-zaya | njaa |
| | | **ny**-uki | **ny**-oshi | nyuki |
| | | **n**-shi | **n**-ntsi | nchi |
| | | | | |
| NG. 10 | n- | **ng**-ozi | **ng**-ozi | ngozi |
| | | **ny**-umba | **ny**-umba | nyumba |
| | | **nj**-aa | **nd**-zaya | njaa |
| | | **ny**-uki | **ny**-oshi | nyuki |
| | | **n**-shi | **n**-ntsi | nchi |
| | | | | |
| NG. 11 | u-<br>Ɵ- | **u**-so | **u**-so | uso |
| | | **u**-limi | **u**-lime | ulimi |
| | | **u**-kucha | **Ɵ**- fuyu | ukucha |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **u**-nyayo | **Ɵ**- haro | unyayo |
| | | **u**-kuta | **u**-hura | ukuta |
| | | | | |
| NG.10/6 | | **ny**-uso | **ny**-iso | uso |
| | | **Ɵ**-ndimi | **Ɵ**-ndimi | ndimi |
| | | **Ɵ**-kucha | **ma**-fuyu | kucha |
| | | **Ɵ**-nyayo | **ma**-haro | nyayo |
| | | **Ɵ**-kuta | **ny**-ihura | kuta |
| NG. 12 | ka-** | - | - | - |
| NG. 13 | tu-** | - | - | - |
| NG. 14 | u- | **u**-rafiki | **u**-wandzani | urafiki |
| | | **u**-zinzi | **u**-zindzi | uzinifu |
| | | **u**-zembe | **u**-laba | uzembe |
| | | **u**-jamaa | **u**-djamaa | ujamaa |
| | | **u**-tumwa | **u**-rumwa | utumwa |
| | | | | |
| NG. 15 | ku-/hu- | **ku**-pika | **hu**-piha | kupika |
| | | **ku**-nwa | **hu**-nywa | kunywa |
| | | **ku**-nya | **hu**-kaka | kunya |
| | | **ku**-fa | **hu**-fa | kufa |
| | | **ku**-kojoa | **hu**-nyawa | kukojoa |
| | | | | |
| NG. 16 | pa- | hapa | dapvanu | hapa |
| | | hapo | dayapvo | hapo |
| | | pale | dapvala | pale |
| | | | | |
| NG. 17 | mu- | humu | dahunu | humu |
| | | humo | dayiho | humo |
| | | mule | dahula | mule |
| | | | | |
| NG. 18 | ku- | huku | Hunu | huku |
| | | huko | Yiho | huko |
| | | kule | Hule | kule |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Tukichunguza Jedwali Na. 1 tunabaini kuwa lahaja ya Kipemba na Kingazija zinafanana katika mfumo wake wa ngeli. Takribani nomino zote za Kipemba na Kingazija zilizobainishwa zina viambishi vya ngeli katika shina la neno. Viambishi hivyo vinashabihiana sana ingawa kuna baadhi vinatofautiana. Aidha, kuna baadhi ya nomino hazina viambishi vya ngeli vilivyo bayana katika maumbo ya umoja au

wingi kama zinavyoonekana katika jedwali hilo. Hata hivyo, Kipemba kina idadi ya ngeli 16 wakati Kingazija kina idadi ya ngeli za nomino ambazo ni 15 kwa kuwa hakina ngeli ya 18. Idadi hiyo imepatikana baada ya kupoteza ngeli ya 12 na 13. Hii ni tofauti na idadi ya ngeli 18 ambazo hubainishwa na waandishi mbalimbali katika Kiswahili sanifu. Hata hivyo, nomino za ngeli ya 12 na 13 zinatokana na athari za Kibantu na bado hazijakubalika moja kwa moja katika Kiswahili sanifu ingawa kuna baadhi ya jamii wanazitumia.

**5.1 Uainishaji wa Ngeli ya 1 na ya 2**

Nomino zilizomo katika kundi hili ni zile zinazotaja viumbe wenye uhai kama vile binadamu, wanyama, wadudu n.k. Nomino za Kipemba na Kingazija zinaundwa na viambishi ngeli vyenye maumbo matatu, yaani 'm/n', 'mu' na 'mw', ambavyo katika umoja na wingi huwakilishwa na 'wa'. Tuangalie mifano ifuatayo:

| **Ngeli** | **Kipemba** | **Kingazija** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|---|
| 1 | **n**-tu | **m**-ndru | mtu |
| | **mu**-umini | **mu**-umini | muumini |
| | **n**-tunke | **mw**-anamshe | mwanamke |
| 2 | **wa**-tu | **wa**-dru | watu |
| | **wa-umini** | wa-umini | waunimini |
| | **wa**-tuwake | **wa**-nawashe | wanawake |

Katika mfano huu tunaona kuwa kiambishi cha ngeli ya kwanza ni 'n' katika Kipemba, na huwa 'm' katika Kingazija. Hii inatokana na sababu kuwa katika Kipemba mara nyingi sauti 'm' hubadilishwa na kuwa 'n' wakati katika Kingazija haibadiliki. Katika mazingira kama hayo, tunaweza kusema kuwa sauti 'n' ya Kipemba imetokana na athari za kifonolojia zilizotokana na wazawa wa lugha yenyewe. Aidha, katika ngeli hiyo, kiambishi 'mu-' huweza kupata sura tofauti zinazoukilia mabadiliko mbalimbali ya kifonolojia, mabadiliko ambayo mara nyingi hutegemea muundo wa shina la nomino zinazohusika. Katika hali kama hiyo, irabu 'u' iliyo katika kiambishi ngeli 'mu-' inapokuwa na ukuruba na irabu ya kwanza ya shina hupata athari za kifonolojia. Hivyo, hali hiyo katika Kipemba na Kingazija imesababisha kiambishi ngeli 'mu-' kuwa na alomofu tatu ambazo ni {mu}, {n} na {mw}. Kadhalika, katika ngeli ya 2, kiambishi 'wa' ambacho kinawakilisha ngeli ya wingi, kimejitokeza katika Kipemba na Kingazija. Hivyo, pamoja na tofauti zilizojitokeza ambazo zimetokana na athari za kifonolojia, kutokana na matumizi ya kiambishi 'n-' badala ya 'm-' katika Kipemba, tunaweza kusema kuwa viambishi vya umoja na wingi katika ngeli ya 1 na ya 2 vimefanana kwa kiasi kikubwa. Kwani kwa mujibu wa Nadharia ya Isimu Historia-Linganishi tofauti hizo za viambishi zimesababishwa na [n] na [m]. Sauti hizo zinahesabiwa kama sauti za aina moja ambazo zinajulikana kama sauti mrejeo.

**5.2 Uainishaji wa Ngeli ya 3 na ya 4**

Katika Jedwali Na. 1 tunaona kuwa viambishi awali vya ngeli ya 3 umoja ni 'm-', 'n-' 'mu-' na 'mw-', ilhali kiambishi awali cha wingi katika ngeli ya 4 ni 'mi-' katika

Kipemba na 'me' katika Kingazija. Aidha, kundi hili hujumuisha nomino mbalimbali zinazohusu miti, sehemu za mwili, hali na vitu vya maumbile, vitu mbalimbali vya matumizi ya kawaida n.k. Tuchunguze baadhi ya ngeli za nomino hizo kama ifuatavyo:

| Ngeli | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| | **n**-ti | **m** -ri | mti |
| 3 | **mu**-ndu | **mu**-ndu | panga |
| | **mw**-ezi | **mw**-ezi | mwezi |
| | **mi**-ti | **mi**-ri | miti |
| 4 | **mi**-ndu | **mi**-ndu | mapanga |
| | **mi-e**zi | **me**zi | miezi |

Mifano iliyo katika Na. 5.2 inadhihirisha kuwa nomino ya kiambishi ngeli ya 3 umoja ni 'mu'. Hivyo, kiambishi hiki katika Kipemba na Kingazija kina alomofu tatu ambazo ni {m}, {n} na {mw}. Alomofu hizi zinatokana na athari za kifonolojia ambapo 'mu-' hubadilika kuwa 'm' na 'n' ikiwa shina la neno linaanza na konsonanti. Vilevile, kiambishi 'mu-' hubadilika kuwa 'mw-' endapo shina la neno litaanza na irabu. Sanjari na hali hiyo, kiambishi cha wingi cha ngeli ya 4 hubadilika kuwa 'mi' katika nomino zote tulizozibainisha hapo juu, isipokuwa katika neno 'mezi' la Kingazija ambalo kiambishi chake cha wingi ni 'me-' badala ya 'mi-'. Kilichojitokeza katika neno hilo, irabu za mbele [i] na [e] zimeungana na kuwa irabu moja tu ambayo ni [e]. Hii ni kanuni ya kawaida sana katika Kiswahili sanifu. Hata hivyo, kanuni hii huwa haifanyi kazi kila wakati kwa sababu kuna baadhi ya mazingira ambayo hayafuati utaratibu huu. Kwa mintarafu hiyo, tunaweza kusema kwamba viambishi vya umoja na wingi katika ngeli ya 3 na ya 4 katika Kipemba na Kingazija vinalandana.

## 5.3 Uainishaji wa Ngeli ya 5 na ya 6

Nomino zinazohusishwa katika kundi la ngeli ya 5 na 6 ni zile zinazohusu viungo vya mwili, vitu vya maumbile n.k. Katika Kipemba na Kingazija viambishi awali vya ngeli ya 5 umoja vimejitokeza katika maumbo yafuatayo: 'ji-', 'gi-', 'di-, 'ja', 'dja'na 'Ɵ-'. Katika ngeli ya 6 viambishi hivyo vinawakilishwa na maumbo 'ma' na 'me'. Hebu tuchunguze viambishi hivyo vilivyojidhihirisha katika nomino zifuatazo:

| Ngeli | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| | **ji**-bwe | Ɵ-bwe | jiwe |
| | Ɵ-shikio | Ɵ-shishiyo | sikio |
| 5 | Ɵ-jani | Ɵ-wani | jani |
| | **gi**-no | **dzi**-nyo | jino |
| | **di**-cho | **dzi**-tso | jicho |
| | **ja**-bali | **dja**-bali | jabali |
| | **ma**-bwe | **ma**-we | mawe |
| 6 | **ma**-shikio | **ma**-shishiyo | masikio |

| | | |
|---|---|---|
| **ma**-jani | **ma**-ni | majani |
| **me**-no | **ma**-nyo | meno |
| **ma**-cho | **ma**-tso | macho |
| **ma**-jabali | **ma**-djabali | majabali |

Katika kipengele Na. 5.3 tunaona kuwa kiambishi awali cha umoja katika ngeli ya 5 kimejibainisha katika maumbo sita kulingana na nomino husika. Mathalani, katika Kingazija kuna udondoshaji wa kiambishi 'ji' katika neno 'bwe' wakati ambapo katika Kipemba kiambishi hicho hakikudondoshwa kama ilivyo katika neno 'jibwe'. Kwa mantiki hiyo, kiambishi awali cha nomino hiyo katika Kipemba kinakuwa ni 'ji-'. Halikadhalika, kuna mabadiliko ya viambishi awali 'gi-', 'di-' na 'ja-' vinavyotumika katika Kipemba kuwa 'dzi-' na 'dja-' katika Kingazija ambapo pia, tumebaini kuwa viambishi 'gi-' na 'di-' vinabadilika kuwa 'dzi-' kama inavyojibainisha katika nomino hizo hapo juu. Aidha, umbo 'Ɵ-' limejitokeza kama kiambishi awali cha ngeli ya umoja katika maneno 'sikio' na 'jani'. Ama kuhusu kiambishi cha wingi katika ngeli ya 6 kimejidhihirisha kama 'ma-' katika nomino zote za Kingazija. Kwa upande wa Kipemba, kiambishi hicho kimejitokeza katika nomino zote isipokuwa nomino moja tu 'meno'. Nomino hiyo imeonekana kupokea mabadiliko ya kifonolojia ambayo tumeyajadili hapo juu (taz. 5.2). Hata hivyo, pamoja na tofauti za hapa na pale za viambishi hivyo, kwa mujibu wa nadharia iliyotumika kuongoza utafiti huu, hivyo vyote ni viambishi vya aina moja. Hii ni kwa sababu viambishi hivyo vimetofautiana sauti tu. Kwa mantiki hiyo, maneno hayo yote ni sawa kwa kuwa yana maana moja. Maneno hayo katika Nadharia ya Isimu Historia-Linganishi yanajulikana kama maneno mnasaba.

**5.4 Uainishaji wa Ngeli ya 7 na ya 8**

Kundi hili linajumuisha nomino mbalimbali kama vile sehemu za mwili, vyakula, vifaa, jumuiya, lugha n.k. Katika makala haya tumebaini viambishi awali vya ngeli ya 7 umoja vya Kipemba na Kingazija kuwa ni: 'ki-/shi', 'ky-/sh-', 'ha-' na 'hi-'. Aidha, viambishi vya wingi vya ngeli ya 8 ni ‘vy-', 'z'-, ‘vi-‘, 'zi-' na 'za-'. Tuchunguze nomino zifuatazo:

| **Ngeli** | **Kipemba** | **Kingazija** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|---|
| | ***ki***-*buno* | ***shi***-*wun* | kiuno |
| 7 | ***ch***-*akulya* | ***sh***-*ahula* | chakula |
| | ***ky***-*uma* | ***sh***-*uma* | chuma |
| | ***ky***-*anwa* | ***h***-*anywa* | kinywa |
| | ***ki***-*chwa* | ***hi***-*tswa* | kichwa |
| | ***ki***-*yazi* | ***shi***-*yazi* | kiazi |
| | ***vy***-*akulya* | ***z***-*ahula* | vyakula |
| 8 | ***vy***-*uma* | ***z***-*uma* | vyuma |
| | ***vi***-*buno* | ***zi***-*wuno* | viuno |
| | ***vi***-*nywa* | ***za***-*nwa* | vinywa |
| | ***vi***-*chwa* | ***zi***-*tswa* | vichwa |
| | ***vi***-*yazi* | ***zi***-*yazi* | viazi |

Tukichunguza nomino zote hizi tunabaini kuwa kiambishi awali 'ki-' cha umoja cha ngeli ya 7 katika Kipemba kimebadilika na kuchukua umbo la kiambishi 'shi-' na 'hi-' katika Kingazija, kwa mfano, nomino *shiwuno* na *hitswa*. Vilevile, viambishi vya Kipemba 'ch-' na 'ky' vimebadili maumbo yake na kuwa 'sh' na 'h' kwa upande wa Kingazija. Mabadiliko haya yametokana na athari za kifonolojia zinazotokana na utamkwaji wa sauti husika. Kipengele hiki tumeshakijadili kwa kina. Katika ngeli ya 8 ambayo inabainisha viambishi vya wingi, viambishi hivyo vimejitokeza katika maumbo mawili 'vy-' na 'vi-' katika Kipemba. Kwa upande wa Kingazija, viambishi hivyo vimejitokeza katika maumbo manne, yaani 'z-', 'za-', zi na 'zu-' kama vinavyoonekana katika nomino *zahuila, zanwa, ziuno* na *zuma*. Hivyo, viambishi hivyo vimeundwa na sauti mrejeo zilizounda maneno mnasaba. Hivyo, mfumo wa ngeli hii unafanana baina ya Kipemba na Kingazija.

**5.5 Uainishaji wa Ngeli ya 9 na ya 10**

Ngeli zinazohusishwa na kundi hili ni zile ambazo viambishi vyake vya umoja na wingi huwa havibadiliki. Mara nyingi kiambishi 'n-' ndicho ambacho kinatumika katika umoja na wakati huohuo hutumika katika wingi. Baadhi ya wataalamu wanadai kuwa huenda kundi hili lilikuwa na kiambishi ngeli 'n-' lakini ama kilipotea au kudondoshwa kihistoria na kuachwa shina pekee katika nomino zisizoanza na kiambishi hiki. Hata hivyo, kuna baadhi ya nomino ambazo huwekwa katika kundi hili kimofolojia lakini zikawekwa katika kundi jingine la ngeli kisintaksia na kisemantiki (Habwe na Karanja, 2012). Mifano ya nomino zinazoingia katika kundi hili ni kama vile nyumba, ndege, miji na mazao. Katika hali ya kawaida, nomino katika ngeli ya 9 na 10 haziwezi kubainishwa katika kigezo cha kimofolojia pekee. Hivyo, ni dhahiri kuwa nomino hizo zinahitaji uamilifu wake wa kisintaksia ili tuweze kuzitenganisha katika umoja na wingi. Tuangalie mifano ifuatayo ya nomino:

| Ngeli | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| | **ng**-ozi | **ng**-ozi | ngozi |
| 9 | **ny**-umba | **ny**-umba | nyumba |
| | **nj**-aa | **nd**-zaya | njaa |
| | **ny**-uki | **ny**-oshi | nyuki |
| | **n**-shi | **n**-ntsi | nchi |
| | **ng**-ozi | **ng**-ozi | ngozi |
| 10 | **ny**-umba | **ny**-umba | nyumba |
| | **nj**-aa | **nd-**zaya | njaa |
| | **ny**-uki | **ny**-oshi | nyuki |
| | **n**-shi | **n**-ntsi | nchi |

Nomino zote zinazoonekana katika ngeli ya 9 na 10 zimejibainisha kuwa na kiambishi 'n-' kwenye maumbo yake yote. Hii ni kudhihirisha kuwa maumbo ya ngeli za nomino katika kundi hili yanafanana baina ya Kipemba na Kingazija.

**5.6 Uainishaji wa Ngeli ya 11**

Mara nyingi nomino zinazohusishwa katika kundi hili huwa na kiambishi 'u-' katika ngeli ya umoja. Kwa kawaida ngeli za kundi hili hupata viambishi vya wingi kutoka katika ngeli ya 10 na ya 6. Nomino zinazohusishwa ni pamoja na baadhi ya nomino za sehemu za viungo vya mwili wa mwanadamu na nomino ambazo hazihesabiki na hivyo haziwezi kuingia katika umoja na wingi, kama vile mafuta, uji, chai, n.k. Tuchunguze baadhi ya nomino hizo:

| Ngeli | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| | **u**-so | **u**-so | uso |
| | **u**-limi | **u**-lime | ulimi |
| 11 | **u**-kucha | Ɵ- fuyu | ukucha |
| | **u**-nyayo | Ɵ- karo | unyayo |
| | **u**-kuta | **u**-hura | ukuta |
| | **ny**-uso | **ny**-iso | nyuso |
| 10/6 | Ɵ-ndimi | Ɵ-ndimi | ndimi |
| | Ɵ-kucha | **ma**-fuyu | kucha |
| | Ɵ-nyayo | **ma**-haro | nyayo |
| | Ɵ-kuta | **ny**-ihura | kuta |

Mifano ya ngeli za nomino katika kundi hili, inaonesha kuwa kiambishi 'u-' ambacho kinawakilisha ngeli ya umoja, kimejitokeza katika baadhi ya nomino za kundi la ngeli ya 11. Hata hivyo, nomino nyingi ambazo zimebainika kuwa na kiambishi hicho, ni zile zinazopatikana katika Kipemba. Hii ni kwa kuwa baadhi ya nomino za Kingazija, zimekengeuka utaratibu huo. Nomino za Kingazija ambazo zimechukua kiambishi ngeli 'u-' ni 'uso', 'ulimi' na 'ukuta' ambapo nomino 'ukucha' na 'unyayo' zimedhihirika kuwa na umbo la 'Ɵ-'. Hata hivyo, kwa kuwa nomino hizo zina maana sawa, zinachukuliwa kama nomino za aina moja kulingana na nadharia iliyotumika katika makala haya.

Kama ambavyo tumetangulia kufafanua (taz. 5.6) kuwa ngeli za kundi hili zinachukua maumbo ya wingi kutoka katika ngeli ya 10 na ya 6. Hivyo, baadhi ya maumbo ya wingi yanayoonekana katika ngeli ya 11, yamebainika kuwa na viambishi ambavyo vimeelemea katika ngeli hizo. Katika Kipemba, neno 'nyuso' limefuata utaratibu wa ngeli ya 10 ambapo kiambishi 'ny-' kimetumika katika neno hilo. Pamoja na utaratibu huo, nomino zote zilizobaki katika Kipemba hazikudhihirisha kuwa na kiambishi 'ny-'. Badala yake zimejibainisha kuwa na kiambishi chenye umbo la 'Ɵ-'. Nomino za wingi katika Kingazija zinaonekana kuegemea katika ngeli zote, ya 10 na ya 6. Kwa mfano, nomino 'nyuso' na 'kuta', zimechukua kiambishi cha wingi 'ny-' cha ngeli ya 10. Wakati huohuo nomino 'kucha' na 'nyayo' zimebainika kuwa na kiambishi cha wingi 'ma' cha ngeli ya 6. Pamoja na hilo, nomino 'ndimi' inajidhihirisha kuwa na kiambishi cha umbo la 'Ɵ-' katika Kipemba na Kingazija.

### 5.7 Uainishaji wa Ngeli ya 14

Maumbo ya nomino katika Kipemba na Kingazija katika ngeli ya 14 yamebainika kuchukua kiambishi 'u-'. Utaratibu wa ngeli hii hujumuisha nomino zinazohusu majina ya vitu, dhana au viumbe vya kufikirika. Vitu hivyo kwa hakika hatuwezi kuvigusa kwa mikono au kuviona kupitia macho yetu. Vilevile, baadhi ya nomino za namna hiyo, mbali na kuwa ni za kufikirika, baadhi yake ni vigumu kuzielewa, kwa kuwa hazina sifa bainifu ambazo tunaweza kuzithibitisha kupitia milango yetu ya fahamu. Zaidi ya hayo, nomino hizo hazibadiliki katika viambishi vyake vya umoja na wingi. Hebu tuangalie mifano ya nomino za aina hii kama ifuatavyo:

| **Ngeli** | **Kipemba** | **Kingazija** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|---|
| | **u**-rafiki | **u**-wandzani | urafiki |
| 14 | **u**-zinzi | **u**-zindzi | uzinifu |
| | **u**-zembe | **u**-laba | uzembe |
| | **u**-jamaa | **u**-djamaa | ujamaa |
| | **u**-tumwa | **u**-rumwa | utumwa |

Nomino zote hizo katika ngeli ya 14 zinaonesha kuwa na kiambishi cha 'u-' ambacho kimepatikana kutokana na shina la nomino, kitenzi na hata kivumishi. Aidha, kiambishi hicho kinabaki kama kilivyo, yaani hakibadiliki katika umoja na wingi kama zilivyo sifa za nomino zenyewe. Hivyo, tunaweza kubaini namna Kipemba kilivyoshabihiana na Kingazija katika maumbo ya nomino ya 14.

### 5.8 Uainishaji wa Ngeli ya 15

Nomino za ngeli ya 15 zinarejelea vitenzi visoukomo vinavyosimama kama nomino. Mara nyingine nomino hizi hujulikana kama vitenzi jina au nomino vitenzi ambapo huathirika kimatumizi. Katika ngeli hii kiambishi chake ni 'ku/hu-' ambacho huwekwa katika shina la kitenzi husika. Nomino zifuatazo zinadhihirisha hali hiyo:

| **Ngeli** | **Kipemba** | **Kingazija** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|---|
| | **ku**-pika | **hu**-piha | kupika |
| 15 | **ku**-nwa | **hu**-nywa | kunywa |
| | **ku**-nya | **hu**-kaka | kufa |
| | **ku**-bauwa | **hu**-nyawa | kukojoa |

Kutokana na mifano ya ngeli hiyo, tunaweza kuona kuwa kiambishi 'ku-' kimejidhihirisha katika ngeli ya 15 katika nomino za Kipemba. Kwa upande wa nomino za Kingazija kiambishi 'ku-' kimebadilika na kuwa 'hu-' kutokana na utaratibu wa lugha husika kwa kuwa kila lugha ina utaratibu wake ambao wanajamii lugha hiyo wanaufuata. Pamoja na kuwapo kwa tofauti hiyo, tunadiriki kusisitiza kuwa viambishi vya ngeli ya 15 katika nomino za Kipemba vimefanana na Kingazija.

### 5.9 Uainishaji wa Ngeli ya 16, 17 na 18

Ngeli za nomino ya 16, 17 na ya 18 zinarejelea hali mbalimbali za mahali na ndiyo maana hujulikana kama ngeli za mahali. Viambishi ambavyo vinapatikana katika ngeli hii ni: 'pa-', 'mu-' na 'ku-'. Tuchunguze mifano ifuatayo:

| Ngeli | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| | ha-**pa** | da-**pvanu** | hapa |
| 16 | ha-**po** | daya-**pvo** | hapo |
| | pa-**le** | da-**pvala** | pale |
| | hu-**m** | da-**hunu** | humu |
| 17 | hu-**mo** | da-**yiho** | humo |
| | mu-**le** | da-**hula** | mule |
| 18 | hu-**ku** | hu-**nu** | huku |
| | hu-**ko** | yi-**ho** | huko |
| | ku-**le** | hu-**le** | kule |

Katika mifano inayojitokeza katika ngeli ya 16, 17 na ya 18 tunaona kuwa viambishi ngeli hubainisha mahali. Ngeli ya 16 kwa kawaida huonesha mahali fulani mahususi palipokusudiwa na msemaji kwa kutumia kiambishi 'pa-'. Katika ngeli ya 17, kiambishi chake cha 'ku-' mara nyingi kinaonesha mahali kwa ujumla wake. Aidha, katika ngeli ya 18 nomino zake huwa zinaonesha mahali ambapo ni ndani kwa kutumia kiambishi 'mu-'. Ndani humo mnaweza kuwa karibu, mbali kidogo au mbali kabisa. Ngeli za nomino katika kundi hili pia, viambishi vyake vya mahali vinaukilia umbali wa masafa uliopo baina ya msemaji na msemeshwaji. Masafa hayo yanaweza kuwa ya karibu, karibu kidogo au ya mbali. Maumbo ya viambishi 'pa', 'mu' na 'ku' yameonekana kujitokeza katika Kipemba. Kwa upande wa Kingazija vimejitokeza kama 'pvanu' badalaya 'pa', 'hunu' badala ya 'mu' na 'nu' badala ya 'ku'. Hii imejitokeza kulingana na utaratibu wa lugha yao. Hata hivyo, maumbo hayo yanawakilisha viambishi vilevile ambavyo ni 'pa' 'mu' na 'ku' vilivyojitokeza katika Kipemba. Hivyo, kwa kiasi kikubwa mfumo wa ngeli za nomino katika Kipemba na Kingazija unalingana.

## 6.0 Hitimisho

Kimofolojia kuna mfanano wa viambishi vya ngeli vinavyopachikwa katika maumbo ya maneno ya Kipemba na Kingazija. Hii inadhihirisha kuwa jamii za wazugumzaji hao kuna wakati ziliwahi kukutana ndiyo maana kukawa na uhusiano huo. Aidha, baadhi ya maneno viambishi vyake vinaonekana kusigana. Hata hivyo, kwa mujibu wa Nadharia ya Isimu Historia-Linganishi iliyotumika katika uchambuzi wa data za makala haya, viambishi hivyo vimejengwa na sauti zinazojulikana kama sauti mrejeo ambazo zinaunda maneno mnasaba[5]. Hivyo,

[5] Upatanishi uliopo baina ya maneno au miundo iliyo na uhusiano wa kiasili, ingawa maumbo au miundo hiyo inaweza kuwa na sura au maumbo yasiyofanana katika umbo nje lake (Massamba, 2004: 52).

tofauti ndogondogo zilizojitokeza katika maumbo hayo zimechombezwa na umbali wa kimasafa uliopo baina ya Kisiwa cha Pemba na Kisiwa cha Ngazija, na hivyo, kuwafanya wazungumzaji lugha zao watofautiane kiuzungumzaji kulingana na mazingira yaliyowazunguka. Aidha, tofauti hizo zinaonesha kuwa jamii za Wapemba na Wangazija baadaye zilitengana kutokana na sababu mbalimbali za kibinadamu kama vile, kutafuta maisha, biashara n.k. Hivyo, tunathubutu kusema kwamba Kipemba na Kingazija zina uhusiano wa kimnasaba kwa sababu zinatokana na mame-lugha moja.

**Marejeleo**

Anttila, R. (1972). *An Introduction to Historical and Comparative Linguistics.* New York: Macmillan Publishing Co. Inc.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili.* Nairobi: Oxford University Press. Macmillan Publisher.

Habwe, J. na Karanja, P. (2012). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Jones, W. (1786). A Dissertation on the Orthography of Asiatick Words in Roman Letters, *katika Asiatick Researches,*1:1-56.

Juma, H.K. (2019). Ulinganishi wa Kihistoria na Kiisimu wa Lahaja za Kiamu, Kimvita, Kipemba, Kitumbatu na Kimicheweni. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Khamis, A.M. na Kiango, J.G. (2002). *Uchanganuzi wa Sarufi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.

Kihore, Y.M., Massamba D.P.B.; Y. P. Msanjila & Kihore Y. (2012). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2017). *Historia ya Kiswahili: Mtazamo Mpya 100KK hadi 2000BK.* Dares Salaam: Kiswahili Development Limited.

Nurse, D. (1989). *Is Comorian Swahili? Being an Examination of the Diachronic Relationship between Comorian and Coastal Swahili*. Paris: Editions Recherche sur les Civilisations.

Nurse, D. na Hinnebusch, T.J. (1993). *Swahili and Sabaki.* California: California University.

Nurse, D. na Spear, T. (1985). *The Kiswahili: Reconstructing the History and Language of an African Society.* Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Swadesh, M. (1952). "Lexicostatistic Dating of Prechistoric Ethnic Contacts". Katika *Preceeding American Philosophical Society,* 96: 452-463.